JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

Simu Na. +255 (026) 2963341/2963346
Nukushi: +255 (026) 2963348
Barua Pepe: ps@jamii.go.tz
Tovuti: **www.jamii.go.tz**

Mji wa Serikali - Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L.P 573,
DODOMA.

14 Septemba, 2023

TAARIFA KWA UMMA

YAH: USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA MKUTANO WA KIPINDI CHA KATI CHA JUKWAA LA KIZAZI CHENYE USAWA UTAKAOFANYIKA JIJI LA NEW YORK, MAREKANI TAREHE 17 SEPTEMBA, 2023.

Wizara inaujulisha Umma wa Watanzania kuwa, Mkutano wa Kimataifa unaojulikana kama Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa '***Generation Equality Forum Mid-Point Conference'*** uliojikita katika kuongeza kasi/chachu ya kufikia Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi utafanyika Jijini New York tarehe 17 Septemba, 2023.

Jukwaa la Kizazi chenye Usawa ni jukwaa la kimataifa lililoitishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake na Usawa wa Jinsia (UN Women) kwa kushirikiana na Serikali za Mexico na Ufaransa. Lengo la jukwaa hili ilikua ni kuharakisha utekelezaji wa ahadi za usawa wa kijinsia zilizopatikana baada ya tathmini ya utekelezaji wa Azimio la Ulingo wa Beijing wakati wa maadhimisho ya miaka 25 ya ulingo huo yaliyobaini kuwepo kwa baadhi ya changamoto ambazo ni vikwazo kufikia usawa wa kijinsia. Vikwazo hivi ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia, mabadiliko ya tabianchi, na mifumo ya kiuchumi ambayo inawaacha nyuma wanawake na wasichana.

Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa mataifa yaliyoshiriki kupitisha na kukubali kutekeleza Haki na Usawa wa Kiuchumi kama njia ya kufikia usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake. Haya ni matamanio ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa awamu ya 6 wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alikubali kuwa kinara wa utekelezaji wake hususan kwenye maeneo ya uwekezaji wenye mlengo wa kijinsia katika huduma na kazi za matunzo kwenye sekta za umma na binafsi; kazi zenye staha kwa wanawake kwenye sekta rasmi na zisizo rasmi; upatikanaji na umiliki wa rasilimali za uzalishaji kwa wanawake; na mipango ya uchumi kwa jumla, maboresho ya kibajeti na vichocheo vya kiuchumi kwa kaya masikini vinavyozingatia jinsia.

Kuelekea Mkutano huu, itafanyika mikutano ya pembezoni (Side events) inayotarajiwa kuwa na washiriki 300 ambao ni waweka ahadi kutoka nchi mbalimbali watakao wasilisha taarifa ya utekelezaji wa nchi kwenye maeneo yao ya ahadi. **Aidha, Malengo mahsusi ya mkutano huo ni pamoja na:**

(i) Kupata taarifa ya utekelezaji na uwajibikaji kwa waweka ahadi na viongozi wa makundi ya watekelezaji;

Mkutano huu utakutanisha watu mbalimbali Duniani ukijumuisha watoa maamuzi kutoka sekta tofauti zikiwemo Serikali, Asasi za kiraia, Sekta binafsi, Mashirika ya kimataifa, Mashirika yanayotetea haki za wanawake ili kujadili na kupata suluhisho la mambo yanayowakabili wanawake na wasichana, kuimarisha utekelezaji na uwajibikaji na kuleta mabadiliko. Aidha, Mkutano utawezesha kuimarisha ushirikiano kuliko ilivyokuwa hapo awali kwa kujenga daraja kati ya watendaji na mitazamo ya watetezi wa haki kutoka nchi mbalimbali.

(ii) Kupanua wigo na kupata waweka ahadi wapya kwa ajili ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa Ahadi za Kizazi chenye Usawa;

Mkutano huu unahamasisha na kukuza nafasi za nchi kushiriki na kuweka ahadi katika eneo la haki na usawa wa kiuchumi ili kuongeza kasi na maarifa ya kufikia usawa wa kijinsia nchini. Vilevile washiriki wa mkutano huu, watakuwa na fursa ya kupata maarifa mapya, ujuzi, na uhusiano utakaosaidia kufikia malengo yao ya utetezi wa haki za wasichana na wanawake. Aidha, kuwatia nguvu mpya waweka ahadi wa makundi mbalimbali ili kuongeza umoja na mshikamano katika utekelezaji wa ahadi hizi ili kufikia usawa wa Jinsia na Uwezeshaji Wanawake kiuchumi.

(iii) Kuchochea jitihada za kimataifa na za nchi.

Mkutano huu unatoa fursa muhimu ya kutathmini Sera na uwajibikaji kulingana na maazimio yaliyofikiwa wakati wa mikutano iliyopita kuhusu usawa wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na Jukwaa la Kizazi chenye Usawa (*Generation Equality Forum* - GEF), Mkutano wa Kimataifa wa Elimu (*The Global Education Summit*), Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (*The United Nations General Assembly* - UNGA), Tume ya Hali ya Wanawake (*Commission on the Status of Women* - CSW), Mkutano wa G7, na Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa (COP26) na mengineyo.

Masuala ya wasichana na wanawake ni mojawapo ya makundi muhimu yanayoratibiwa na Wizara ninayoongoza. Takwimu za Duniani zinaonesha kuwa Wanawake ni takriban billioni **3.99** na kwa Tanzania, idadi ya wanawake ni million **31.67** kulingana na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka ***2022***.

Aidha, Serikali inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** inawatambua na kuwajali wanawake kwa kufanya juhudi za kuhakikisha changamoto zao zinatatuliwa. Vilevile, Mheshimiwa Rais ni Kinara wa Haki na Usawa wa Kiuchumi katika utekelezaji wa Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa ambapo lengo ni kuwezesha usawa wa wanawake na wanaume kushiriki kikamilifu kwenye masuala ya uchumi kwa ustawi wa familia na Taifa kwa ujumla. Jitihada ambazo Serikali imekuwa ikitekeleza ni pamoja na:

i. Kuundwa kwa Wizara mahsusi ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inayoweka kipaumbele eneo la usawa wa kijinsia;

ii. Kuteuliwa kwa Kamati ya Taifa ya Ushauri yenye wajumbe 25 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakijumuisha wataalam wa sekta mbalimbali kutoka Tanzania Bara Zanzibar. Kamati hiyo inaongozwa na mwenyekiti **Mhe. Angela Kairiki (Mb),** Waziri wa Maliasili na Utalii;

iii. Kuundwa kwa Program ya Kizazi chenye Usawa Tanzania (*Tanzania Generation Equality Programme* - TGEP) inayotekelezwa na Wizara za kisekta kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia Julai 2021/22 hadi Juni 2025/26 yenye mkakati madhubuti unaolenga kuleta mabadiliko ya ubora wa maisha ya wanawake na wasichana wa Kitanzania kwa kuimarisha Haki na Usawa wa Kiuchumi pasipo kuwaacha nyuma wanaume na wavulana kwa kuwajengea uelewa ili waweze kushiriki kwenye maendeleo ya Taifa.

iv. Kuteuliwa kwa maafisa viungo kuanzi ngazi ya Halmashauri, Sekretarieti za Mikoa na Wizara wenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa haki na usawa wa kiuchumi kwenye maeneo yao; na

v. Kuitambua Siku ya Wanawake Duniani sambamba na kushirikiana na Wadau kushughulikia changamoto za wanawake kama ilivyobainishwa katika Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 pamoja na Mpango wa Mkakati wake wa mwaka 2005; Maazimio ya Ulingo wa Beijing, Ajenda ya Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Ajenda ya Maendeleo ya Bara la Afrika 2063.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali yakiwemo Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa, Asasi za Kiraia, Wanaharakati na Sekta Binafsi nchini itashiriki mkutano huu wa kipindi cha kati cha utekelezaji wa Jukwaa la Kizazi chenye Usawa.

Napenda kuwajulisha kwamba, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania <u>ameniteua nimwakilishe kwenye Mkutano huo</u> ambapo, matukio muhimu yatakuwa yafuatayo:-

1. Tarehe 16 Septemba, 2023 ni mkutano wa pembeni wa unaojikita katika ushirikishwaji wa vijana katika kizazi chenye usawa Pamoja na mkutano wa pembezoni wa wadau wa asasi za kiraia wanaotekeleza kizazi chenye usawa (*Generation Equality Civil Society stakeholders*).
2. Tarehe 17 Septemba, 2023 kutakuwa na tukio kubwa ambalo ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa kipindi cha kati cha kizazi chenye usawa (generation equality forum) ambapo nchi mbalimbali zinazotekeleza generation equality zitapata fursa ya kuelezea utekelezaji wake ;
3. Tarehe 18 Septemba, 2023 kutakuwa na mkutano wa pembeni wa *United Republic of Tanzania on Generation Equality Localization* ambapo Tanzania itapata nafasi ya kuwasilisha taarifa zenye mfumo wa makala na video zinazoonyesha hali halisi ya utekelezaji wa kizazi chenye usawa;
4. Tarehe 20 Septemba, 2023 kutakuwa na Mkutano kuhusu Programu ya Malezi na Makuzi (ECD) itakayofanyika kwenye makao makuu ya United Nations - New York;

Ujumbe wa Tanzania utajumuisha ushiriki wa Mashirika mbalimbali yaliyoweka jitihada katika kukuza usawa na uwezeshaji wa wanawake. Mashirika hayo ni pamoja na Shirika la Kimataifa UN women; Benki ya NMB na Asasi ya Nakua na Taifa Langu.

Mwisho, naomba kutumia fursa hii kuendelea kuwasihi waandishi wa habari na wadau wote kuungana na Serikali kufichua ukiukwaji wa haki kwa Wasichana na Wanawake ili haki itendeke, pia kuongeza juhudi zaidi kukabiliana na vitendo vya ukatili, unyanyasaji na kuwainua wanawake wapate uwezo wa kiuchumi wa kuzihudumia familia zao. **Nina imani mtaendelea kufuatilia yanayojiri New York - Marekani na kuwapa taarifa wananchi wa Tanzania kuhusu yanayojadiliwa kwa kuinua hali na haki za wanawake na wasichana kote nchini.**

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika

Imetolewa na

Dkt. Dorothy Gwajima (**Mb**).

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM